# MALAIKA

# YESU

# MUNGU

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  MALAIKA,YESU NA MUNGU.Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MALAIKA,YESU NA MUNGU

1.Malaika…………………………………………………………

2. Yesu…………………………………………………………..

3. Mungu………………………………………………………..

4. Makao ya Mbinguni……………………………………….

5.Kuokoka…………………………………………………………….

6. Mwisho…………………………………………………………

# 1. MALAIKA?

Malaika ni ni wenyeji  wa mbinguni kwa Baba yake Yesu yaani mungu wenye umbo kama mwanadamu wenye nuru  na nguvu za mungu baadhi ni wajumbe wa mungu na walinzi hutumwa kwa watumishi wa mungu au Yesu  aliowatuma au kuwapeleka kutoa ujumbe au injili au  kuwalinda watumishi wa mungu na kazi ya Mungu.

Ee mtu wa  Kimaitaifa uliyeokoka u mchanga kiroho sipendi ukose ufahamu juu ya malaika usiwe mgeni ktk wokovu ikiwa umejaliwa neema ya kuwaona  Mfano ktk mbingu ya Tanzania wapo wa aina tatu ninaowafahamu:=>

**1) Full suit ya Njano**

Hawa ni Malaika wenye nuru ya njano kuanzia kichwani mpaka miguni unaweza usione ngozi ya miili yao ila wakizima nuru yao wakakuonesha ngozi ya miili ni ya pekee kama ya Yesu (Wazungu) na wanazungukwa na utaji wa nuru kama ya njano kuanzianzia kichwani hadi miguuni.

**2)Full suit ya Bluu**

Hawa ni malaika wenye nuru ya rangi ya bluu

**3)Full suit ya Rangi ya ganda la Zabibu (Blue + Weusi)**

Hawa ni malaika wenye nuru ya rangi ya ganda la zabibu   wana rangi ya Nyeusi iliyochanganyikana blue  kuanzia  Kichwani mpaka miguuni Hawakupi haki ya kuona ngozi ya miili yao  labda wakujalie neema.

Malaika wapo watiifu kwa Mungu ktk ile kazi ya mungu waliyotumwa. Mfano malaika ulinzi wao wapo kwa kulinda kazi ya mungu na watumishi wa mungu usitafute ujumbe au injili kwa watumishi wa mungu hutapata. Malaika waliobeba injili ya mungu wapo kwa ajili ya injili. Malaika wa Mungu hubeba habari njema za Mungu na Yesu.

## 2.YESU?

Unataka kufahamu ulipookoka Yesu yu ndani yako na wewe u ndani yake. Utamtambua kazi zake na maisha yenye ushuhuda ya bila kutenda dhambi yanaanza kutenda kazi ndani yako. Yesu alivyo kwa kazi zake ni mponyaji,mtenda miujiza au maajabu,Ana Amri ya kutoa Pepo,Mwenye Kufungua waliofungwa,Mwenye kufundisha mambo ya Ufalme wa Mbinguni,Mwenye Kubariki,Ni Nabii na anayechukia uovu au dhambi ni mwenye hake.Yesu kama umeokoka hukupa hiyo ya kuchukia dhambi na moja au zaidi ya kazi zake kwa alichhokutabiria uliyeoka kama wewe mtu wa kimataifa kutoa pepo kwa jina lake,kuponya wagonjwa,Kutenda miujiza.

Neema kumwonaa Yesu hutegemea na kusudi la mungu kwako na Huduma aliyokupa na utegemea Moyo safi.

**Mathayo** 5:8 "Heri wenye **moyo safi;** Maana hao watamwona **Mungu.** "

Yesu ni mwana wa mungu ni mungu pia mfano mwanakondoo ni kondoo yaani mtoto wa kondoo ni kondoo si mbuzi.Wote wenye Moyo safi wa neema ya kuona Yesu. Ukitaka kumwona yesu penda mafundisho ya yesu uwe hodari kuyatenda utakuwa na moyo safi.

Watumishi wa Yesu wa huduma za kanisa zifuatazo hupewa neema ya kumwona Yesu:=>

1) **Mitume:** Mitume 12 walimuona Yesu kuishi na kufundishwa naye Mtume alimwona Yesu juu ya mbinguni juu ya dunia wakati anaitwa alipofuka macho kwa sababu alikuwa mwenye dhambi nakusikia sauti iliyosema Sauli!Sauli mbona waniudhi akauliza ni nani wewe Yesu alisema ni mimi Yesu.
2) **Mwalimu wa kanisa la waliokoka.** Mwalimu Paulo ambaye mwanzo aliitwa sauli.
3) **Mhubiri:** Mhubiri Paulo ambaye mwanzo aliitwa sauli.

## 3. MUNGU

Mungu ni muumbaji.  Aliumba vyote vinavyoonekana na Visivyoneekana. Mfano soma Kitabu cha Mwanzo ktk Biblia; wanyama,dunia,mwanadamu,mimea,jua, nuru, nyota, mwenzi,samaki na bahari,miti ya matunda mbalimbali.

Huyo mungu muumbaji Yesu tunayemwamini na kumfuata anamwitwa Baba. Yesu ni Mtoto wa Kiume wa Mungu.

Je Mungu ni anaonekana huyo alituumba? Jibu ndiyo

**Mathayo 5:8** "Heri wenye **moyo safi;** Maana hao watamwona **Mungu.** "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka unaweza kumuona mungu ukiwa na **Moyo safi** peke kwa wazi zaidi usafi wa ufikie kiwango wa Yesu unapewa kibali cha mungu wakati. Lakini wale wote waliomwona Yesu na alama zake za misumari ktk miguu na mikono na kwenye ubavu wamemwona mungu muumbaji yaani baba yake Yesu.

**Yohana 14:7— 11**

"...Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.

Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? **Aliyeniona** mimi amemwona **Baba;** basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? …"

Mifano wa waliomwona Baba yake Yesu ni Yakobo **(Mwanzo 32:24-30),** Nabii Musa(**kutoka 33:18-23),** Mtume Yohana.**(ufunuo wa Yohana 4).**

Unabii unatoka kwa yaani Baba yake Yesu **2Petro 1: 21** Manabii wakubwa ndio huweza kupewa neema ya kumwona  Mungu yaani Baba Yesu

## 4. MAKAO YA MBINGUNI

Makao ya mbinguni ni mahali alipoandaa Yesu mbinguni kwa Baba yake kwa ajili kuishi na watakatifu wake waliokoka baada kufa miaka 2000 iliyopita ukianza na mitume nakanisa la mwanzo ktk matendo ya mitume ukianza Stefano shahidi aliokoka na kuuwa kwa ajili ya imani yake kwa bwana Yesu mbele ya Sauli alipookoka alitwa Mtume,Mwalimu na Mhubiri Paulo ndiye aliyeingia makao matakatifu.

Kabla ya Yesu kufa na kufufuka aliwaahidi mitume na wote watakao mtumikia kuwa pamoja mahali alipo na aliwaambia anakwenda kuandaa makao na kuishi na hao watakaomtumikia kwa uamini kama Bwana baada ya Maisha haya au kufa ataishi nao ktk makao ya mbinguni.

**Yohana 14 : 2 - 3**

"Nyumbani mwa Baba yangu mna **makao** mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia **mahali.**

Basi mimi nikienda na kuwaandalia **mahali,** nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo. "

**Yohana 12 : 26** " Mtu **akinitumikia,** na anifuate; nami nilipo, ndipo na **mtumishi** wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu. "

Yesu baada kufufuka yupo mbinguni ktk makao matakatifu aliwaanda kuishi na wale watakaomtumikia waliokoka wanaomkiri ni Bwana na mwokozi wenye tumini na kufufuliwa mungu aliyemfufua yeye baada kifo.Ukitaka ukweli wa makao aliyoandaa yesu jinsi kulivyo Yesu alimwonesha mwandishi wake alitokea kati 1994 –2000 na kumchukua mpaka mbinguni na kumwonesha kisha kumtuma kuandika kitabu cha makao aliyoandaa kinachoitwa **KWELI MBINGU IPO** na **Mwandishi wa CHOO NAM.** Tafuta kitabu hiki ukakisome upate kufahamu baada kifo utaishi sehemu nzuri sana.

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034